# MATUKIO YA UKATILI NA UDHALILISHAJI WA KIJINSIA KWA MWAKA 2023









April, 2024

United Nations Entity for Gender Equality and the Empowerment of Women

**OFISI YA MTAKWIMU MKUU WA SERIKALI ZANZIBAR**

# TAKWIMU ZA UKATILI NA UDHALILISHAJI WA KIJINSIA KWA MWAKA 2023

# YALIYOMO


DIBAJI....................................................................................................ii

MUHTASARI..........................................................................................iv

MISAMIATI.............................................................................................v

VIFUPISHO...........................................................................................vi

SEHEMU A: WILAYA YA KASKAZINI“A”..................................................1

SEHEMU B: WILAYA YA KASKAZINI“B”..................................................8

SEHEMU C: WILAYA YA KATI.............................................................16

SEHEMU D: WILAYA YA KUSINI..........................................................23

SEHEMU E: WILAYA YA MJINI.............................................................30

SEHEMU F: WILAYA YA MAGHARIBI “A”..............................................37

SEHEMU G: WILAYA YA MAGHARIBI “B”..............................................44

SEHEMU H: WILAYA YA WETE ...........................................................51

SEHEMU I: WILAYA YA MICHEWENI....................................................58

SEHEMU J: WILAYA YA CHAKECHAKE.................................................65

SEHEMU K: WILAYA YA MKOANI.........................................................72

# DIBAJI

Kitabu cha Takwimu za Udhalilishaji wa Kijinsia ni chanzo muhimu cha habari inayowasilisha takwimu kwa mwaka 2023. Takwimu hizi hutolewa kila mwezi na Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali (OCGS) kupitia vyombo vya habari. Ripoti hii imetokana na takwimu zinazoripotiwa katika vituo vya Polisi vya wilaya za Zanzibar na kujumuishwa kwa pamoja Makao Makuu ya Polisi Zanzibar. Lengo kuu la ripoti hii ni kutoa taarifa za ukatili na udhalilishaji wa kijinsia za ndani ya Zanzibar. Taarifa hizi hutumiwa na wapangaji, watunga sera, na watoa maamuzi.

OCGS inatoa shukurani zake za dhati kwa UN WOMEN wote walioshiriki katika kutoa chapisho hili. Kwa namna ya kipekee inatanguliza shukrani zake Makao Makuu ya Polisi, Zanzibar kwa ushirikiano wa kutupatia taarifa hizi. Vilevile, inamshukuru Ndugu Fahima M. Issa kwa kuratibu chapisho hili pamoja na wataalam wa kiufundi wafuatao: Sabina R. Daima Mkuu wa Divisheni ya Takwimu za Jinsia na Ajira, Ramla H. Pandu , Asha M. Mahfoudh na Ahmada H. Suleiman watakwimu wa divisheni ya Jinsia na Ajira kwa kujitolea kwao na kushiriki kikamilifu katika uandaaji wa ripoti ya udhalilishaji Zanzibar.

OCGS inakaribisha maoni kutoka kwa watumiaji sio tu kwenye takwimu zilizotolewa na ubora wake lakini pia kutoa mapendekezo yatakayosaidia kuboresha takwimu zetu kwa toleo lijalo.



.....................................................................

**Salum Kassim Ali**

**Mtakwimu Mkuu wa Serikali**

**Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali, Zanzibar.**

**Kwa maelezo zaidi wasiliana na:**

**Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali**

**S.L.P. 2321, Zanzibar**

**7 Barabara ya Fumba,**

**71125 Mjini Magharibi**

**Zanzibar – Tanzania**

**Simu: +255 24 224 0134**

**Nukushi: +255 24 224 0135**

**Baruapepe: cgs@ocgs.go.tz**

**Tovuti:www.ocgs.go.tz.**

# MUHTASARI

Kitabu hichi ni muendelezo wa vitabu vya Takwimu za Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia Zanzibar ambapo kitabu cha kwanza kilitolewa 2020 na Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali na kinatarajiwa kuendelea kutolewa kila mwaka. Kitabu hiki kinatoa muhtasari wa takwimu za maeneo mawili ya uhalifu ambayo ni ukatili na udhalilishaji wa Kijinsia kwa kila wilaya kwa mwaka 2023. Takwimu hizi zimechambuliwa kijiografia, kimakundi na kijinsi kwa wilaya zote 11 za Unguja na Pemba. Data hukusanywa kila mwezi kutoka Makao Makuu ya Polisi na matokeo haya kuwasilishwa katika vyombo vya habari kila mwezi.

Chapisho hili hutoa taarifa za ukatili na udhalilishaji wa kijinsia Zanzibar. Vilevile hutoa taarifa za idadi ya matukio yaliyotokea, aina ya waathirika na hali ya waathirika baada ya ukatili na udhalilishaji wa kijinsia. Takwimu hizi hutoa taarifa kuhusu matukio ambayo yameainishwa katika makundi makuu sita (6) ambayo ni Kubaka, Kulawiti na Kunajisi, Kuingilia kinyume na maumbile, Kutorosha, Shambulio la aibu/kukashifu na Shambulio na inatafsiriwa kwa kutofautiana na jinsi ya muaathirika.

## MISAMIATI

1. **Kubaka:** Tendo hili linahusisha wanawake na wasichana
2. **Kulawiti/Kunajisi:** Tendo hili linahusisha wanaume na wavulana tu.
3. **Kuingilia kinyume na maumbile:** Tendo hili linahusisha wanawake na wasichana tu.
4. **Kutorosha:** Tendo hili linahusisha wanawake, wasichana, wanaume na wavulana.
5. **Shambulio la aibu /Kukashifu:** Tendo hili linahusisha wanawake, wasichana, wanaume na wavulana (Mfano kumgusa sehemu za siri bila ya ridhaa yake, kumtukana matusi ya nguoni nk).
6. **Shambulio:** Tendo hili linahusisha wanawake, wasichana, wanaume na wavulana tu.

**Angalizo:**

**Wasichana:** watoto wa kike wenye umri chini ya mikaka 18.

**Wanawake:** watu wazima wanawake wenye miaka 18 na zaidi.

**Wavulana**: watoto wa kiume wenye umri chini ya miaka 18.

**Wanaume:** watu wazima wenye umri wa miaka 18 na zaidi.

# VIFUPISHO

| | |
|---|---|
| Apr | Aprili |
| Dis | Disemba |
| Jan | Januari |
| Jml | Jumla |
| Okt | Oktoba |
| Sept | Septemba |
| W'k | Wanawake |
| W's | Wasichana |
| W'v | Wavulana |
| W'u | Wanaume |

## Idadi ya Matukio na Waathirika wa Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia

| Wilaya | Idadi ya Matukio | Idadi ya Waathirika | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | | Wanawake | Wanaume | Wasichana | Wavulana |
| Jumla | 1,954 | 236 | 84 | 1,263 | 376 |
| Kaskazini “A” | 98 | 21 | 0 | 66 | 11 |
| Kaskazini “B” | 113 | 19 | 1 | 78 | 15 |
| Kati | 94 | 12 | 0 | 67 | 15 |
| Kusini | 45 | 8 | 0 | 30 | 7 |
| Mjini | 457 | 60 | 35 | 252 | 110 |
| Magharibi “A” | 433 | 53 | 28 | 276 | 76 |
| Magharibi “B” | 417 | 37 | 19 | 268 | 93 |
| Wete | 93 | 5 | 1 | 63 | 24 |
| Micheweni | 42 | 1 | 0 | 36 | 5 |
| Chakechake | 108 | 13 | 0 | 81 | 19 |
| Mkoani | 54 | 7 | 0 | 46 | 1 |

# WILAYA ZA ZANZIBAR






SHEHIA ZA WILAYA YA KASKAZINI A




## Idadi ya Watu

Kwa mujibu wa Sensa ya Watu na Makazi ya mwaka 2022, Wilaya ya Kaskazini “A” ilikuwa na Idadi ya watu 157,369 kati yao, wanawake walikuwa watu 80,205 (asilimia 51.0) na wanaume ni watu 77,164 (asilimia 49.0), Watoto walioko chini ya miaka 17 ni 71,084 ambao ni sawa na asilimia 45.2, watu wenye miaka 18 na zaidi ni 86,285 sawa na asilimia 54.8, Jadweli A.1.

**Jadweli A.1: Idadi ya Watu wa Wilaya ya Kaskazini "A" kwa Umri na Jinsi; 2022**




*Chanzo: Idadi ya Watu na Makaazi, 2022*

## Matukio ya Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia

Jumla ya matukio 98 ya ukatili na udhalilishaji wa kijinsia yameripotiwa katika Wilaya ya Kaskazini "A" mwaka wa 2023, Waathirika wengi walikuwa ni watoto ambao ni 77 sawa na asilimia 78.6 na wanawake ni 21 sawa na asilimia 21.4 (Jadweli A.11).

Robo ya nne ya mwaka 2023 (Oktoba-Disemba) imeripotiwa kuwa na matukio mengi zaidi ambayo yalikuwa matukio 29 (asilimia 29.6) ikilinganishwa na vipindi vyengine, aidha robo mwaka ya Aprili-Juni imeripotiwa kuwa na matukio kidogo (matukio 20 sawa na silimia 20.4), Kielelezo A.1.

### Kielelezo A.1: Idadi ya Matukio ya Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia kwa Vipindi vya Robo Mwaka; 2023




Matukio ya udhalilishaji wa wasichana ndio yanayoongoza zaidi katika wilaya ya Kaskazini "A" kwa mwaka 2023, ambapo wameripotiwa waathirika 66 (asilimia 67.4) ikifuatia na matukio ya udhalilishaji wa wanawake ikiwa na waathirika 21 (asilimia 21.4) na kwa wavulana walikuwa waathirika 11 (asilimia 11.2) Kielelezo A. 2.

### Kielelezo A.2: Idadi ya Waathirika wa Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia kwa Jinsi; 2023




Wasichana wanaonekana kuathirika zaidi ambapo kati ya waathirika 98 wasichana ni 66. Vile vile katika vipindi vyote vya robo mwaka inaonekana wasichana ndio waathirika zaidi ambapo robo mwaka ya kwanza waathirika wasichana walikuwa 17 kati ya 23, robo mwaka ya pili na ya tatu walikuwa 16 kati ya waathirika 20 na 25 mtawaliwa, na robo mwaka ya nne walikuwa waathirika 17 kati ya 29. Kielelezo A.3.

**Kielelezo A3: Idadi ya Waathirika wa Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia kwa Vipindi vya Robo mwaka na Jinsi; 2023**




Udhalilishaji mkubwa unaofanyika kwa wanawake na wasichana ni ubakaji ambapo kati ya matukio 87 ya udhalilishaji yaliyotokea kwa wanawake na wasichana, Kati ya matukio 59 yaliyotokea ya  ni kubaka likifuatia na shambulio la aibu /kukashifu yalkuwa matukio 10, kutorosha yalikuwa matukio manane (8), shambulio yalikuwa sita (6) na kuingilia kinyume na maumbile yaliripotiwa matukio manne (4). Kielelezo A.4.

**Kielelezo A.4: Idadi ya Matukio ya Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia kwa Wanawake na Wasichana kwa Aina ya Matukio; 2023**




Kati ya matukio 59 yaliyotokea ya kubaka, 49 walifanyiwa wasichana na matukio 10 walifanyiwa wanawake. Matukio mengine yote yanaonekana kufanyiwa zaidi wasichana ukilinganisha na wanawake isipokuwa matukio ya shambulio yote yaliripotiwa kufanyiwa wanawake (matukio 6), Kielelezo A.5.

### Kielelezo A.5: Idadi ya Matukio ya wa Udhalilishaji wa Kijinsia kwa Wanawake na Wasichana kwa Aina ya Matukio na Jinsi; 202




Kwa upande wa wavulana, matukio yaliyoripotiwa yalikuwa ni kulawiti (matukio 11) ambapo matukio wengine matatu ya udhalilishaji hayakuripotiwa katika wilaya hii (Kielelezo A.6).

### Kielelezo A.6: Idadi ya Matukio ya Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia kwa Wavulana kwa Aina ya Matukio; 2023



## Kiambatisho

### Jadweli A.11: Idadi ya Waathirika wa  Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia kwa Jinsi; 2023

| Waathirika | Idadi | Asilimia |
|---|---|---|
| Wanawake | 21 | 21.4 |
| Watoto | 77 | 78.6 |

### Jadweli A.12: Idadi ya Matukio ya Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia kwa Wanawake na Wasichana kwa Vipindi vya robo mwaka, Aina ya Matukio na Jinsi; 2023

| Aina ya Matukio | Jan - Machi | | | Apr - Juni | | | Julai - Sept | | | Okt - Dis | | | Jan - Dis | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | W'k | W's | Jml | W'k | W's | Jml | W'k | W's | Jml | W'k | W's | Jml | W'k | W's | Jml |
| Kubaka | 1 | 16 | 17 | 1 | 8 | 9 | 2 | 13 | 15 | 6 | 12 | 18 | 10 | 49 | 59 |
| Kuingilia kinyume na maumbile | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 1 | 1 | 2 | 3 | 1 | 3 | 4 |
| Kutorosha | 0 | 1 | 1 | 0 | 4 | 4 | 0 | 1 | 1 | 0 | 2 | 2 | 0 | 8 | 8 |
| Kukashifu/shambulio la aibu | 0 | 0 | 0 | 0 | 4 | 4 | 2 | 1 | 3 | 2 | 1 | 3 | 4 | 6 | 10 |
| Shambulio | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 1 | 5 | 0 | 5 | 0 | 0 | 0 | 6 | 0 | 6 |
| **Jumla** | **1** | **17** | **18** | **2** | **16** | **18** | **9** | **16** | **25** | **9** | **17** | **26** | **21** | **66** | **87** |

## Jadweli A.13: Idadi ya Matukio ya Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia kwa Wavulana kwa Vipindi vya Robo Mwaka na Aina ya Matukio; 2023

| Aina ya udhalilishaji | Jan - Machi | Apr - Juni | Julai - Sept | Okt - Dis | Jan - Dis |
|---|---|---|---|---|---|
| Kulawiti | 5 | 2 | 1 | 3 | 11 |
| Kutorosha | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Kukashifu/Shambulio la aibu | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Shambulio | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| **Jumla** | **5** | **2** | **1** | **3** | **11** |

## Jadweli A.14: Hatua Zilizochukuliwa kwa Aina ya Matukio; 2023

| Aina ya Matukio | Idadi ya Matukio | Idadi ya Waathirika | | | | Zinazoendelea Mahakamani | Zilizopata hatia | Zilizochini ya Upelelezi | Zilizopelekwa kwa DPP | Zilizoondolewa Mahakamani | Zilizofungwa Polisi |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | W'k | W's | W'v | W'u | | | | | | |
| Kubaka | 59 | 10 | 49 | | | 30 | 10 | 7 | 5 | 4 | 3 |
| Kulawiti | 11 | | | 11 | 0 | 5 | 4 | 2 | 0 | 0 | 0 |
| Kuingilia kinyume na maumbile | 4 | 1 | 3 | | | 3 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 |
| Kutorosha | 8 | 0 | 8 | 0 | 0 | 1 | 1 | 6 | 0 | 0 | 0 |
| Shambulio la aibu/Kukashif | 10 | 4 | 6 | 0 | 0 | 7 | 0 | 3 | 0 | 0 | 0 |
| Shmabulio | 6 | 6 | 0 | 0 | 0 | 2 | 1 | 3 | 0 | 0 | 0 |
| **Jumla** | **98** | **21** | **66** | 11 | **0** | **48** | **16** | **22** | **5** | **4** | **3** |

## SEHEMU B: WILAYA YA KASKAZINI “B”




### Idadi ya Watu

Idadi ya watu kwa Wilaya ya Kaskazini “B” kwa mwaka 2022 walikuwa watu 99,921. Wanawake walikuwa 50,744 (asilimia 50.8) na wanaume 49,177 (asilimia 49.2), Watoto walioko chini ya miaka 17 ni 46,682 sawa na asilimia 46.7, watu wenye miaka 18 na zaidi ni 53,239 sawa na asilimia 53.3, Jadweli B.1.

### Jadweli B.1: Idadi ya Watu wa Wilaya ya Kaskazini “B” kwa Umri na Jinsi; 2022




*Chanzo: Sensa ya Watu na Makazi, 2022*

## Matukio ya Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia

Jumla ya matukio 113 ya ukatili na udhalilishaji wa kijinsia yameripotiwa katika Wilaya ya Kaskazini “B” kwa mwaka wa 2023. Waathirika wengi walikuwa watoto (watoto 93 sawa na asilimia 82.3), wanawake waathirika ni 19 sawa na asilimia 16.8 na mwanamme mmoja (1) sawa na asilimia 0.9(Jadweli B.11).

Robo ya tatu na ya nne ya mwaka 2023 (Julai – Septemba na Oktoba - Disemba) zimeripotiwa kuwa na matukio mengi zaidi ambayo yalikuwa matukio 31 kwa kila kipindi sawa na asilimia 27.4 ikilinganishwa na vipindi vyengine na robo ya mwaka.

Aprili - Juni imeripotiwa kuwa na matukio kidogo ambayo ni 25 sawa na asilimia 22.1, Kielelezo B.1.

**Kielelezo B.1: Idadi ya Matukio ya Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia kwa Vipindi vya Robo mwaka; 2023**




Matukio ya udhalilishaji kwa wasichana yanayoongoza zaidi katika Wilaya ya Kaskazini" B". Waathirika wasichana walikuwa 78 sawa na asilimia 69.0 waliripotiwa ikifuatia na matukio ya udhalilishaji wa wanawake waathirika walikuwa 19 (asilimia 16.8), mwanamme alikuwa mmoja (1) sawa na asilimia 0.9 na wavulana walikuwa 15 (asilimia 13.3), Kielelezo B.2.

**Kielelezo B.2: Idadi ya Waathirika wa Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia kwa Jinsi; 2023**




Wasichana wameonekana kuathirika zaidi ambapo kati ya waathirika 113, wasichana walikuwa 78. Vile vile katika vipindi vyote vya robo mwaka inaonekana wasichana ndio waathirika zaidi ambapo robo mwaka ya kwanza kulikuwa na waathirika 17 kati ya 26, robo mwaka ya pili waathirika 15 kati ya 25, robo mwaka ya tatu waathirika 25 kati ya 31 na robo mwaka ya nne wasichana 21 kati ya 31. Kielelezo B.3.

## Kielelezo B.3: Idadi ya Waathirika wa Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia kwa Vipindi vya Robo mwaka na Jinsi; 2023




Udhalilishaji mkubwa unaofanyika kwa wanawake na wasichana ni ubakaji ambapo kati ya matukio 97 ya udhalilishaji yaliyotokea kwa mwaka 2023 kwa wanawake na wasichana, matukio 74 yalikuwa ni kubaka likifuatia matukio ya shambulio la aibu / kukashifu ambayo yalikuwa matukio 14, Kielelezo B.4.

## Kielelezo B.4: Idadi ya Matukio ya Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia kwa Wanawake na Wasichana kwa Aina ya Matukio; 2023



Kati ya waathirika 74 wa matukio ya kubaka, 66 walifanyiwa wasichana na matukio manane (8) walifanyiwa wanawake. Matukio mengine yote yanaonekana kufanyiwa zaidi wasichana ukilinganisha na wanawake isipokuwa tukio la shambulio, Kielelezo B.5.

**Kielelezo B.5: Idadi ya Matukio wa Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia kwa Wanawake na Wasichana kwa Aina ya Matukio; 2023**




Kwa upande wa wavulana na wanaume matukio yanayoongoza zaidi ni kulawiti yameripotiwa matukio 15 yote walifanyiwa wavulana likifuatia tukio la shambulio la aibu/kukashifu limeripotiwa tukio moja (1) kwa wanaume ambapo matukio mengine hayakuripotiwa kwa wavulana na wanaume (Kielelezo B.6).

**Kielelezo B.6: Idadi ya Matukio ya Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia kwa Wavulana kwa Aina ya Matukio; 2023**



## Kiambatanisho

### Jadweli B.11: Idadi ya Waathirika wa  Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia kwa Jinsi; 2023

| Waathirika | Idadi | Asilimia |
|---|---|---|
| Wanawake | 19 | 16.8 |
| Wanaume | 1 | 0.9 |
| Watoto | 93 | 82.3 |

### Jadweli B.12: Idadi ya Matukio ya Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia kwa Wanawake na Wasichana kwa Vipindi vya Robo mwaka, Aina ya Matukio na Jinsi; 2023

| Aina ya Matukio | Jan - Machi | | | Apr - Juni | | | Julai - Sept | | | Okt - Dis | | | Jan - Dis | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | W'k | W's | Jml | W'k | W's | Jml | W'k | W's | Jml | W'k | W's | Jml | W'k | W's | Jml |
| Kubaka | 2 | 13 | 15 | 1 | 13 | 14 | 0 | 21 | 21 | 5 | 19 | 24 | 8 | 66 | 74 |
| Kuingilia kinyume na maumbile | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Kutorosha | 0 | 1 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 1 |
| Kukashifu/shambulio la aibu | 1 | 3 | 4 | 1 | 1 | 2 | 0 | 3 | 3 | 3 | 2 | 5 | 5 | 9 | 14 |
| Shambulio | 1 | 0 | 1 | 4 | 1 | 5 | 1 | 1 | 2 | 0 | 0 | 0 | 6 | 2 | 8 |
| **Jumla** | **4** | **17** | **21** | **6** | **15** | **21** | **1** | **25** | **26** | **8** | **21** | **29** | **19** | **78** | **97** |

## Jadweli B.13: Idadi ya Matukio ya Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia kwa Wavulana na Wanaume kwa Vipindi vya Robo mwaka na Aina ya Matukio; 2023

| Aina ya Matukio | Jan - Machi | | | Apr - Juni | | | Julai - Sept | | | Okt - Dis | | | Jan - Dis | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | W'v | W'u | Jml | W'v | W'u | Jml | W'v | W'u | Jml | W'v | W'u | Jml | W'v | W'u | Jml |
| Kulawiti | 5 | 0 | 4 | 0 | 4 | 0 | 2 | 0 | 15 | 0 | 5 | 0 | 4 | 0 | 4 |
| Kutorosha | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Kukashifu/shambulio la aibu | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Shambulio | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| **Jumla** | **5** | **0** | **4** | **0** | **4** | **1** | **2** | **0** | **15** | **1** | **5** | **0** | **4** | **0** | **4** |

## Jadweli B.14: Hatua Zilizochukuliwa kwa Aina ya Matukio; 2023

| Aina ya Matukio | Idadi ya Matukio | Idadi ya Waathirika | | | | Zinazoendelea Mahakamani | Zilizopata hatia | Zilizochini ya Upelelezi | Zilizopelekwa kwa DPP | Zilizoondolewa Mahakamani | Zilizofungwa Polisi |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | W'k | W's | W'v | W'u | | | | | | |
| Kubaka | 74 | 8 | 66 | | | 39 | 14 | 11 | 7 | 3 | 0 |
| Kulawiti | 15 | | | 15 | 0 | 11 | 1 | 3 | 0 | 0 | 0 |
| Kuingilia kinyume na ma-umbile | 0 | 0 | 0 | | | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Kutorosha | 1 | 0 | 1 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Shambulio la aibu/Kukashif | 15 | 5 | 9 | 0 | 1 | 9 | 2 | 4 | 0 | 0 | 0 |
| Shmabulio | 8 | 6 | 2 | 0 | 0 | 3 | 1 | 4 | 0 | 0 | 0 |
| **Jumla** | **113** | **19** | **78** | **15** | **1** | **63** | **18** | **22** | **7** | **3** | **0** |

SHEHIA ZA WILAYA YA KATI




## Idadi ya Watu

Sensa ya Watu na Makazi ya mwaka 2022 ilionyesha Idadi ya watu wa wilaya ya Kati walikuwa watu 132,717.  Wanawake walikuwa watu 66,148 (asilimia 49.7) na wanaume walikuwa 66,569 (asilimia 50.3). Mchanganuo wa makundi ya umri umeonyesha kuwa watoto walioko chini ya miaka 17 ni watu 59,716 sawa na asilimia 45.0, watu wenye miaka 18 na zaidi walikuwa watu 73,001 sawa na asilimia 55.0, Jadweli C.1.

**Jadweli C.1: Idadi ya Watu wa Wilaya ya Kati kwa Umri na Jinsi; 2022**




*Chanzo: Sensa ya Watu na Makazi, 2022*

## Matukio ya Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia

Jumla ya matukio 94 ya ukatili na udhalilishaji wa kijinsia yameripotiwa katika mwaka wa 2023, waathirika wengi walikuwa watoto (watoto 82 sawa na asilimia 87.2) na wanawake waathirika walikuwa 12 sawa na asilimia 12.8(Jadweli C.11).

Robo mwaka ya pili ya mwaka 2023 (Aprili – Juni) imeripotiwa kuwa na matukio mengi, matukio 37 (asilimia 39.4) ikilinganishwa na vipindi vyengine vya robo mwaka ambapo kipindi cha Januari - Machi imeripotiwa kuwa na matukio kidogo zaidi, matukio 18 sawa na asilimia 19.1, Kielelezo C.1.

**Kielelezo C.1: Idadi ya Matukio ya Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia kwa robo mwaka; 2023**




Matukio ya udhalilishaji kwa wasichana ndio yanayoongoza zaidi katika Wilaya ya Kati, waathirika 67 (asilimia 71.4) walikuwa wasichana ikifuatia na matukio ya udhalilishaji kwa wavulana walikuwa waathirika 15 na udhalilishaji kwa wanawake walikuwa waathirika, Kielelezo C.2.

**Kielelezo C.2: Idadi ya Waathirika wa Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia kwa Jinsi; 2023**




Wasichana wameonekana kuathirika zaidi ambapo kati ya waathirika 94, wasichana 67 wameathirika. Vile vile katika vipindi vyote vya robo mwaka inaonekana wasichana ndio waathirika zaidi ambapo robo mwaka ya kwanza kulikuwa na waathirika wasichana 12 kati ya 18, robo mwaka ya pili waathirika 29 kati ya 37, robo mwaka ya tatu waathirika 11 kati ya 19 na robo mwaka ya nne waathirika wasichana 15 kati ya 20. Kielelezo C.3.

**Kielelezo C.3: Idadi ya Waathirika wa Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia kwa robo mwaka na Jinsi; 2023**




Udhalilishaji mkubwa unaofanyika kwa wanawake na wasichana ni ubakaji ambapo kati ya matukio 79 ya udhalilishaji yaliyotokea, matukio 51 yalikuwa ni kubaka likifuatia tukio la kuingilia kinyume na maumbile ambayo yalikuwa matukio 16. Kielelezo C.4.

**Kielelezo C.4: Idadi ya Matukio ya Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia kwa Wanawake na Wasichana kwa Aina ya Matukio; 2023**




Kati ya matukio 51 yaliyotokea ya kubaka, 43 walifanyiwa wasichana na matukio nane (8) walifanyiwa wanawake. Matukio mengine yote yanaonekana kufanyiwa zaidi wasichana ukilinganisha na wanawake, Kielelezo C.5.

## Kielelezo C.5: Idadi ya Matukio wa Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia kwa Wanawake na Wasichana kwa Aina ya Matukio; 2023




Kwa upande wa wavulana, tukio la kulawiti linaongoza zaidi ambapo matukuio 13 yameripotiwa. Tukio la kukashifu/shambulio la aibu yameripotiwa matukio mawili (2) ambapo matukio mengine hayakuripotiwa katika wilaya hii (Kielelezo C.6).

## Kielelezo C.6: Idadi ya Matukio ya Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia kwa Wavulana kwa Aina ya Matukio; 2023



## Kiambatanisho

### Jadweli C.11: Idadi ya Waathirika wa  Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia kwa Jinsi; 2023

| Waathirika | Idadi | Asilimia |
|---|---|---|
| Wanawake | 12 | 12.8 |
| Watoto | 82 | 87.2 |

### Jadweli C.12: Idadi ya Matukio ya Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia kwa Wanawake na Wasichana kwa Vipindi vya Robo mwaka, Aina ya Matukio na Jinsi; 2023

| Aina ya Matukio | Jani - Machi | | | Apr - Juni | | | Julai - Sept | | | Okt - Dis | | | Jan - Dis | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | W'k | W's | Jml | W'k | W's | Jml | W'k | W's | Jml | W'k | W's | Jml | W'k | W's | Jml |
| Kubaka | 3 | 10 | 13 | 3 | 18 | 21 | 1 | 5 | 6 | 1 | 10 | 11 | 8 | 43 | 51 |
| Kuingilia kinyume na maumbile | 0 | 2 | 2 | 0 | 8 | 8 | 0 | 5 | 5 | 0 | 1 | 1 | 0 | 16 | 16 |
| Kutorosha | 0 | 0 | 0 | 0 | 2 | 2 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 1 | 0 | 3 | 3 |
| Kukashifu/shambulio la aibu | 0 | 0 | 0 | 1 | 1 | 2 | 3 | 1 | 4 | 0 | 3 | 3 | 4 | 5 | 9 |
| Shambulio | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| **Jumla** | **3** | **12** | **15** | **4** | **29** | **33** | **4** | **11** | **15** | **1** | **15** | **16** | **12** | **67** | **79** |

## Jadweli C.13: Idadi ya Matukio ya Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia kwa Wavulana kwa Vipindi vya Robo mwaka na Aina ya Matukio; 2023

| Aina ya udhalilishaji | Jan - Machi | Apr - Juni | Julai - Sept | Okt - Dis | Jan - Dis |
|---|---|---|---|---|---|
| Kulawiti | 3 | 4 | 3 | 3 | 13 |
| Kutorosha | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Kukashifu/Shambulio la aibu | 0 | 0 | 1 | 1 | 2 |
| Shambulio | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| **Jumla** | **3** | **4** | **4** | **4** | **15** |

## Jadweli C.14: Hatua Zilizochukuliwa kwa Aina ya Matukio; 2023

| Aina ya Matukio | Idadi ya Matukio | Idadi ya Waathirika | | | | Zinazoendelea Mahakamani | Zilizopata hatia | Zilizochini ya Upelelezi | Zilizopelekwa kwa DPP | Zilizoondolewa Mahakamani | Zilizofungwa Polisi |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | W'k | W's | W'v | W'u | | | | | | |
| Kubaka | 51 | 8 | 43 | | | 21 | 9 | 11 | 6 | 4 | 0 |
| Kulawiti | 13 | | | 13 | 0 | 7 | 3 | 3 | 0 | 0 | 0 |
| Kuingilia kinyume na ma-umbile | 16 | 0 | 16 | | | 11 | 1 | 3 | 1 | 0 | 0 |
| Kutorosha | 3 | 0 | 3 | 0 | 0 | 0 | 1 | 2 | 0 | 0 | 0 |
| Shambulio la aibu/Kukashif | 11 | 4 | 5 | 2 | 0 | 4 | 6 | 1 | 0 | 0 | 0 |
| Shmabulio | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| **Jumla** | **94** | **12** | **67** | **15** | **0** | **43** | **20** | **20** | **7** | **4** | **0** |

## SEHEMU D: WILAYA YA KUSINI

SHEHIA ZA WILAYA YA KUSINI




## Idadi ya Watu

Idadi ya watu katika Wilaya ya Kusini kwa mwaka 2022 walikuwa watu 63,156 ambapo wanawake walikuwa 31,358 (asilimia 49.7) na wanaume 31,798 (asilimia 50.3). Watoto walio chini ya miaka 17 ni 24,110 sawa na asilimia 38.2, watu wenye miaka 18 na zaidi ni 39,046 sawa na asilimia 61.8, Jadweli D.1.

**Jadweli D.1: Idadi ya Watu wa Wilaya ya Kusini kwa Umri na Jinsi; 2022**




*Chanzo: Sensa ya Watu na Makazi, 2022*

## Matukio ya Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia

Matukio 45 ya ukatili na udhalilishaji wa kijinsia yameripotiwa katika Wilaya ya Kusini mwaka wa 2023, wengi wa waathirika ni watoto ambao ni 37 sawa na asilimia 82.2 na wanawake waathirika walikuwa 8 sawa na asilimia 17.8(Jadweli D.11).

Robo ya nne ya mwaka 2023 (Oktoba - Disemba) imeripotiwa kuwa na matukio mengi (matukio 16) sawa na asilimia 35.6 ikilinganishwa na vipindi vyengine. Robo mwaka ya pili ya Aprili - Juni imeripotiwa kuwa na matukio kidogo, matukio sita (6) sawa na asilimia 13.3. Kielelezo D.1.

**Kielelezo D.1: Idadi ya Matukio ya Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia kwa Vipindi vya Robo mwaka; 2023**




Idadi kubwa ya waathirika wa udhalilishaji wa kijinsia ni wasichana (waathirika 30 sawa na asilimia 66.7) ikifuatiwa na waathirika wanawake (waathirika nane (8)). Idadi ndogo ya waathirika iliripotiwa kwa wavulana a mbapo walikuwa waathirika saba (7) sawa na (asilimia 15.6), Kielelezo D.2.

**Kielelezo D .2: Idadi ya Waathirika wa Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia kwa Jinsi; 2023**



Waathirika wengi ni wasichana ambapo kati ya waathirika 45, waathirika 30 walikuwa wasichana. Hali hii imeonekana pia katika vipindi vyote vya robo mwaka ambapo wasichana ndio waathirika zaidi. Robo mwaka ya kwanza kulikuwa na wasichana waathirika 6 kati ya 9, robo mwaka ya pili waathirika sita (6) kati ya sita (6), robo mwaka ya tatu waathirika 10 kati ya 14 na robo mwaka ya nne waathirika wasichana 8 kati ya 16. Kielelezo D.3.

**Kielelezo D.3: Idadi ya Waathirika wa Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia kwa Vipindi vya Robo mwaka na Jinsi; 2023**




Udhalilishaji mkubwa unaofanyika kwa wanawake na wasichana ni ubakaji ambapo kati ya matukio 43 ya udhalilishaji yaliyotokea kwa wanawake na wasichana, matukio 25 yalikuwa ni kubaka likifuatia tukio la shambulio la aibu / kukashifu ambayo yalikuwa matukio nane (8), Kielelezo D.4.

**Kielelezo D.4: Idadi ya Matukio ya Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia kwa Wanawake na Wasichana kwa Aina ya Matukio; 2023**



Kati ya waathirika 25 wa matukio ya kubaka, 20 walifanyiwa wasichana na matukio 5 walifanyiwa wanawake. Matukio mengine yanaonekana kufanyiwa zaidi wasichana ukilinganisha na wanawake. Kielelezo D.5

### Kielelezo D.5: Idadi ya Matukio wa Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia kwa Wanawake na Wasichana kwa Aina ya Matukio; 2023




Kwa upande wa wavulana tukio la kulawiti linaongoza zaidi (matukio manne (4)) ikifuatia tukio la kukashifu/shambulio la aibu (matukio matatu (3)) ambapo matukio mengine hayakuripotiwa (Kielelezo D.6).

### Kielelezo D.6: Idadi ya Matukio ya Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia kwa Wavulana kwa Aina ya Matukio; 2023



## Kiambatanisho

### Jadweli D.11: Idadi ya Waathirika wa  Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia kwa Jinsi; 2023

| Waathirika | Idadi | Asilimia |
|---|---|---|
| Wanawake | 8 | 17.8 |
| Watoto | 37 | 82.2 |

### Jadweli D.12: Idadi ya Matukio ya Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia kwa Wanawake na Wasichana kwa Vipindi vya Robo mwaka, Aina ya Matukio na Jinsi; 2023

| Aina ya Matukio | Jan - Machi | | | Apr - Juni | | | Julai - Sept | | | Okt - Dis | | | Jan - Dis | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | W'k | W's | Jml | W'k | W's | Jml | W'k | W's | Jml | W'k | W's | Jml | W'k | W's | Jml |
| Kubaka | 1 | 3 | 4 | 0 | 4 | 4 | 1 | 9 | 10 | 3 | 4 | 7 | 5 | 20 | 25 |
| Kuingilia kinyume na maumbile | 0 | 1 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 1 | 2 | 1 | 2 | 3 |
| Kutorosha | 0 | 1 | 1 | 0 | 1 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 2 | 2 |
| Kukashifu/shambulio la aibu | 0 | 1 | 1 | 0 | 1 | 1 | 1 | 1 | 2 | 1 | 3 | 4 | 2 | 6 | 8 |
| Shambulio | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| **Jumla** | **1** | **6** | **7** | **0** | **6** | **6** | **2** | **10** | **12** | **5** | **8** | **13** | **8** | **30** | **38** |

## Jadweli D.13: Idadi ya Matukio ya Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia kwa Wavulana kwa Vipindi vya Robo mwaka Aina ya Matukio; 2023

| Aina ya udhalilishaji | Jani - Machi | Apr - Juni | Julai- Sept | Okt - Dis | Jan - Dis |
|---|---|---|---|---|---|
| Kulawiti | 1 | 0 | 0 | 3 | 4 |
| Kutorosha | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Kukashifu/Shambulio la aibu | 1 | 0 | 2 | 0 | 3 |
| Shambulio | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| **Jumla** | **2** | **0** | **2** | **3** | **7** |

## Jadweli D.14: Hatua Zilizochukuliwa kwa Aina ya Matukio; 2023

| Aina ya Matukio | Idadi ya Matukio | Idadi ya Waathirika | | | | Zinazoendelea Mahakamani | Zilizopata hatia | Zilizochini ya Upelelezi | Zilizopelekwa kwa DPP | Zilizoondolewa Mahakamani | Zilizofungwa Polisi |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | W'k | W's | W'v | W'u | | | | | | |
| Kubaka | 25 | 5 | 20 | | | 8 | 11 | 4 | 2 | 0 | 0 |
| Kulawiti | 4 | | | 4 | 0 | 1 | 0 | 3 | 0 | 0 | 0 |
| Kuingilia kinyume na ma-umbile | 3 | 1 | 2 | | | 1 | 1 | 1 | 0 | 0 | 0 |
| Kutorosha | 2 | 0 | 2 | 0 | 0 | 0 | 0 | 2 | 0 | 0 | 0 |
| Shambulio la aibu/Kukashif | 11 | 2 | 6 | 3 | 0 | 6 | 4 | 1 | 0 | 0 | 0 |
| Shmabulio | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| **Jumla** | **45** | **8** | **30** | **7** | **0** | **16** | **16** | **11** | **2** | **0** | **0** |

SHEHIA ZA WILAYA YA MJINI




## Idadi ya Watu

Idadi ya watu katika Wilaya ya Mjini kwa mwaka 2022 walikuwa watu 219,007 ambapo wanawake walikuwa 113,119 (asilimia 51.7) na wanaume walikuwa 105,888 (asilimia 48.3). Watoto walioko chini ya miaka 17 ni 84,694 sawa na asilimia 38.7, watu wenye miaka 18 na zaidi ni 134,313 sawa na asilimia 61.3, Jadweli E.1.

**Jadweli E.1: Idadi ya Watu wa Wilaya ya Mjini kwa Umri na Jinsi; 2022**




*Chanzo: Sensa ya Watu na Makazi, 2022*

## Matukio ya Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia

Matukio 457 ya ukatili na udhalilishaji wa kijinsia yameripotiwa Wilaya ya Mjini kwa mwaka 2023, wengi wa waathirika walikuwa ni watoto ambao ni 362 (asilimia 79.2), waathirika wanawake walikuwa 60 (asilimia 13.1) na wanaume walikuwa 35 sawa na asilimia 7.7(Jadweli E.11).

Robo ya nne ya mwaka 2023 (Oktoba – Disemba) kumeripotiwa kuwa na matukio mengi zaidi ambayo yalikuwa matukio 135 (asilimia 29.5) ikilinganishwa na vipindi vyengine, aidha, robo mwaka ya Aprili – Juni kumeripotiwa kuwa na matukio kidogo zaidi ambayo ni matukio 93 sawa na asilimia 20.4, Kielelezo E.1.

**Kielelezo E.1: Idadi ya Matukio ya Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia kwa Vipindi vya Robo mwaka; 2023**




Matukio ya Udhalilishaji kwa wasichana ndio yanayoongoza zaidi katika Wilaya ya Mjini ambapo walikuwa waathirika 252 (asilimia 55.1) ikufuatia na wavulana walikuwa 110 (asilimia 24.1), wanawake walikuwa 60 (asilimia 13.1) na kwa wanaume ni 35 sawa na asilimia 7.7, Kielelezo E.2.

**Kielelezo E.2: Idadi ya Waathirika wa Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia kwa Jinsi; 2023**




Waathirika 252 walikuwa wasichana kati ya waathirika 457. Aidha, wasichana ndio waathirika zaidi katika vipindi vyote vya robo mwaka ambapo robo mwaka ya kwanza kulikuwa waathirika 65 kati ya 107, robo mwaka ya pili waathirika 50 kati ya 93, robo mwaka ya tatu waathirika 67 kati ya 122 na robo mwaka ya nne waathirika wasichana 70 kati ya 135. Kielelezo E.3.

**Kielelezo E.3: Idadi ya Waathirika wa Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia kwa Vipindi vya Robo mwaka na Jinsi; 2023**




Udhalilishaji mkubwa unaofanyika kwa wanawake na wasichana ni ubakaji ambapo yalikuwa matukio 179 kati ya matukio 312 ya udhalilishaji yaliyotokea kwa wanawake na wasichana, likifuatia tukio la shambulio ambayo yalikuwa matukio 75. Kielelezo E.4.

**Kielelezo E.4: Idadi ya Matukio ya Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia kwa Wanawake na Wasichana kwa Aina ya Matukio; 2023**




Kati ya matukio 179 yaliyotokea ya kubaka, 155 walifanyiwa wasichana na matukio 24 walifanyiwa wanawake. Matukio mengine yote yanaonekana kufanyiwa zaidi wasichana ukilinganisha na wanawake, Kielelezo E.5

**Kielelezo E.5: Idadi ya Matukio ya Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia kwa Wanawake na Wasichana kwa Aina ya Matukio; 2023**




Kwa upande wa wavulana na wanaume, tukio la kulawiti linaongoza zaidi (matukio 63) ambapo matukio 60 yameripotiwa kwa wavulana na matukio matatu yameripotiwa kwa wanaume likifuatia tukio la shambulio ambapo yameripotiwa matukio 82(matukio 50 yaliripotiwa kwa wavulana na matukio 32 yaliripotiwa kwa wanaume, (Kielelezo E.6).

**Kielelezo E.6: Idadi ya Matukio ya Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia kwa Wavulana na Wanaume kwa Aina ya Matukio; 2023**



## Kiambatanisho

### Jadweli E.11: Idadi ya Waathirika wa  Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia kwa Jinsi; 2023

| Waathirika | Idadi | Asilimia |
|---|---|---|
| Wanawake | 60 | 13.1 |
| Wanaume | 35 | 7.7 |
| Watoto | 362 | 79.2 |

### Jadweli E.12: Idadi ya Matukio ya Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia kwa Wanawake na Wasichana kwa Vipindi vya Robo mwaka, Aina ya Matukio na Jinsi; 2023

| Aina ya Matukio | Jan - Machi | | | Ap r- Juni | | | Julai - Sept | | | Okt - Dis | | | Jan - Dis | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | W'k | W's | Jml | W'k | W's | Jml | W'k | W's | Jml | W'k | W's | Jml | W'k | W's | Jml |
| Kubaka | 2 | 47 | 49 | 5 | 33 | 38 | 8 | 35 | 43 | 9 | 40 | 49 | 24 | 155 | 179 |
| Kuingilia kinyume na maumbile | 0 | 2 | 2 | 0 | 0 | 0 | 0 | 2 | 2 | 1 | 4 | 5 | 1 | 8 | 9 |
| Kutorosha | 1 | 2 | 3 | 0 | 6 | 6 | 1 | 3 | 4 | 0 | 6 | 6 | 2 | 17 | 19 |
| Kukashifu/shambulio la aibu | 1 | 3 | 4 | 2 | 3 | 5 | 3 | 13 | 16 | 0 | 5 | 5 | 6 | 24 | 30 |
| Shambulio | 6 | 11 | 17 | 5 | 8 | 13 | 8 | 14 | 22 | 8 | 15 | 23 | 27 | 48 | 75 |
| **Jumla** | **10** | **65** | **75** | **12** | **50** | **62** | **20** | **67** | **87** | **18** | **70** | **88** | **60** | **252** | **312** |

## Jadweli E.13: Idadi ya Matukio ya Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia kwa Wavulana na Wanaume kwa Vipindi vya Robo mwaka Aina ya Matukio; 2023

| Aina ya Matukio | Jani - Machi | | | Apr - Juni | | | Julai - Sept | | | Okt- Dis | | | Jan - Dis | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | W'v | W'u | Jml | W'v | W'u | Jml | W'v | W'u | Jml | W'v | W'u | Jml | W'v | W'u | Jml |
| Kulawiti | 14 | 2 | 14 | 1 | 10 | 0 | 22 | 0 | 60 | 3 | 14 | 2 | 14 | 1 | 10 |
| Kutorosha | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Kukashifu/shambulio la aibu | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Shambulio | 12 | 4 | 8 | 8 | 15 | 10 | 15 | 10 | 50 | 32 | 12 | 4 | 8 | 8 | 15 |
| **Jumla** | **26** | **6** | **22** | **9** | **25** | **10** | **37** | **10** | **110** | **35** | **26** | **6** | **22** | **9** | **25** |

## Jadweli E.14: Hatua Zilizochukuliwa kwa Aina ya Matukio; 2023

| Aina ya Matukio | Idadi ya Matukio | Idadi ya Waathirika | | | | Zinazoendelea Mahakamani | Zilizopata hatia | Zilizochini ya Upelelezi | Zilizopelekwa kwa DPP | Zilizoondolewa Mahakamani | Zilizofungwa Polisi |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | W'k | W's | W'v | W'u | | | | | | |
| Kubaka | 179 | 24 | 155 | | | 78 | 57 | 39 | 5 | 0 | 0 |
| Kulawiti | 63 | | | 60 | 3 | 25 | 17 | 21 | 0 | 0 | 0 |
| Kuingilia kinyume na maumbile | 9 | 1 | 8 | | | 4 | 1 | 4 | 0 | 0 | 0 |
| Kutorosha | 19 | 2 | 17 | 0 | 0 | 6 | 5 | 8 | 0 | 0 | 0 |
| Shambulio la aibu/Kukashif | 30 | 6 | 24 | 0 | 0 | 12 | 3 | 12 | 3 | 0 | 0 |
| Shmabulio | 157 | 27 | 48 | 50 | 32 | 71 | 15 | 70 | 1 | 0 | 0 |
| **Jumla** | **457** | **60** | **252** | **110** | **35** | **196** | **98** | **154** | **9** | **0** | **0** |

## SEHEMU F: WILAYA YA MAGHARIBI “A”




### Idadi ya Watu

Idadi ya watu wa Wilaya ya Magharibi “A” mwaka 2022 walikuwa watu 329,645, kati ya hao wanawake walikuwa 171,145 (asilimia 51.9) na wanaume walikuwa 158,500 (asilimia 48.1). Watoto wenye umri chini ya miaka 17 walikuwa 156,045 sawa na asilimia 43.3, watu wenye miaka 18 na zaidi walikuwa 173,600 sawa na asilimia 52.7, Jadweli Jadweli F.1.

## Jadweli F.1: Idadi ya Watu wa Wilaya ya Magharibi “A” kwa Umri na Jinsi; 2022




*Chanzo: Sensa ya Watu na Makazi, 2022*

### Matukio ya Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia

Jumla ya matukio 433 ya ukatili na udhalilishaji wa kijinsia yameripotiwa katika wilaya ya Magharibi “A” kwa mwaka wa 2023, wengi wa waathirika walioripotiwa walikuwa watoto ambao ni 352 sawa na asilimia 81.3, waathirika wanawake walikuwa 53 sawa na asilimia 12.2 na wanaume walikuwa 28 sawa na asilimia 6.5 (Jadweli F.11).

Robo ya kwanza ya mwaka 2023 (Januari – Machi) imeripotiwa kuwa na idadi kubwa ya matukio ambayo yalikuwa matukio 122 (asilimia 28.2) ikilinganishwa na vipindi vyengine vya robo mwaka. Aprili - Juni kumeripotiwa kuwa na matukio idadi kidogo, matukio 90 sawa na asilimia 20.8, Kielelezo F.1.

**Kielelezo F.1: Idadi ya Matukio ya Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia kwa Vipindi vya robo mwaka; 2023**




Matukio ya udhalilishaji kwa wasichana ndio yanayoongoza zaidi katika wilaya ya Magharibi "A", waathirika 276 (asilimia 63.7) ikifuatia na udhalilishaji kwa wavulana waathirika 76, kwa wanawake walikuwa 53 (asilimia 12.2) na wanaume walikuwa 28 sawa na asilimia 6.5, Kielelezo F.2.

**Kielelezo F.2: Idadi ya Waathirika wa Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia kwa Jinsi; 2023**




